**MAFUNDISHO YA BIBILIA**
**KWA WATOTO WA**
**KANISA LA ELOHIM (C. O. G)**
**SIKU YA SABA (7TH DAY)**
**ROBO YA KWANZA, 2025**
**JANUARY , FEBRUARY , MARCH**
**KUTUMIWA NA BIBLIA TUMA MAOMBI YOTE KWA**
**3RD ANGEL MESSENGER**
**S. L. P 9774 NAKURU**
**3rdangelmessenger@gmail.com**
**SIMU: +254 721576325 / +254 780976325**

----------------------------------------------------------------

**SOMO LA WATOTO LA JANUARY 4,2025**
**UUMBAJI**
**Somo kuu: Mwanzo 1:1-31**
**Fungu la kukariri: Mwanzo 1:1**

1. Nani aliziumba mbingu na nchi? Mwanzo 1:1.
2. Nini Elohim aliumba siku ya kwanza? Mwanzo 1:4-5.
3. Nini Elohim aliumba siku ya tatu? Mwanzo 1:9-13.
4. Ni-lini Elohim alimuumba mwanadamu? Mwanzo 1:26-31.
5. Baada ya uumbaji, Elohim alifanya nini ? Mwanzo 2:1-2.
6. Je,Elohim alipumzika baada ya uumbaji kwa kuwa alikuwa amechoka? Isaiya 40:28 upatanishe na Kutoka 20:8.
7. Nina aliwapea wanyama Majina yao baada ya uumbaji? Mwanzo 1:20.

**SOMO LA WATOTO LA JANUARY 11, 2025**
**DHAMBI**

**Somo kuu : Warumi 6:1-23**
**Fungu la kukariri : 1 Yohana 3:4**

1. Dhambi ni nini? 1 Yohana 3:4
2. Ni nini Mshahara wa dhambi? Warumi 6:23

3. Je, watenda dhambi wataridhi Ufalme wa Elohim? 1 Wakorintho 6:9-10
4. Elohim alimwambia Kaini nini kuhusu dhambi? Mwanzo 4:7
5. Kwa nini Elohim aliwaangamiza wenyeji wa Sodom na Gomorrah? Mwanzo 13:13, 19:1-25
6. Ayubu alinena vipi kuhusu dhambi? Ayubu 10:6
7. Ni nini kitafanyika kwa watenda dhambi? Waebrania 10:26-27

**SOMO LA WATOTO LA JANUARY 18, 2025**
**AMRI YA TANO**
**Somo kuu: Kutoka 20:1-17**
**Fungu la kukariri : Kutoka 20:12**

1. Ni Amri ipi ya Kwanza yenye ahadi? Waefeso 6:1-2
2. Ni ahadi ipi? Waefeso 6:3
3. Ni vipi inastahili kumchukulia mtu mwenye umri sawa au mzee kuliko baba yetu mzazi?

1 Timotheo 5:1(sehemu ya Kwanza).
4. Ni vipi inastahili kumchukulia mtu mwenye umri sawa au mzee kuliko mama yetu mzazi?
1 Timotheo 5:2(sehemu ya Kwanza).
5. Tukitii wszazi wetu, je yaonyesha twampenda Elohim? Yohana 14:15

6. Je,Masihi aliitii amri hii alipokuwa mtoto? Luka 2:51
7. Ni vingumu kuitunza amri hii? 1 Yohana 5:3

**SOMO LA WATOTO LA JANUARY 25, 2025**
**AMRI YA SITA**
**Somo kuu : Kutoka 20:1-17**
**Fungu la kukariri : Kutoka 20:13**

1. Amri ya Sita, inatuamuru nini? Kutoka 20:13
2. Nani alituamuru tusiue? Kutoka 20:1-13
3. Masihi alinena vipi kuhusu amri hii? Mathayo 5:21-22
4. Yohana yule mtume alinena vipi kuhusu amri hii? 1 Yohana 3:15
5. Mtu akiwa muuaji, baba yake ni nani? Yohana 8:44
6. Ili tusiwe wauaji, twafaa tufanye nini? Yohana 13:34
7. Je,muuaji ana uzima wa milele ndani yake? 1 Yohana 3:15

**SOMO LA WATOTO LA FEBRUARY 1, 2025**
**AMRI YA TISA**
**Somo kuu : Kutoka 20:1-20**
**Fungu la kukariri : Kutoka 20:16**

1. Nani alipeana Amri kumi? Kutoka 20:1-3
2. Amri ya tisa inatukataza tusifanye nini? Kutoka 20:16
3. Ni nini shahidi wa uongo atafanya? Mithali 14:5
4. Je, shahidi wa uongo ataadhibiwa? Mithali 19:5
5. Mwandishi wa Zaburi amenena vipi kuhusu shahidi wa uongo? Zaburi 27:12
6. Ni nini imesemwa kuhusu Mtu yule ambaye anashuhudia uongo jirani yake?

1. Mithali 25:18

7. Ni wapi ushuhuda wa uongo hutoka? Mathayo 15:19

**SOMO LA WATOTO LA FEBRUARY 8, 2025**
**MAOMBI**
**Somo kuu: Mathayo 6:1-21**
**Fungu la kukariri : 1 Wathesalonike 5:17**

1. Ushauri wa Paulo kuhusu maombi ni upi? Wakolosai 4:2,1 Wathesalonike 5:17
2. Tuombapo tumeshauriwa tufanye vipi? 1 Wakorinitho 14:15
3. Je, Paulo aliwaambia ndugu wengine wamkumbuke katika maombi Yao? Wakolosai 4:3
4. Je,Danieli aliogopa kuomba Elohim baada ya mfalme kutoa agizo la kwambai mtu yeyote
asimuombe Elohim? Danieli 6:10
5. Ni ombi lipi Masihi aliwafunza wafuasi wake? Mathayo 6:9-13
6. Tunapo omba nini tumeshauriwa tusifanye? Mathayo 6:5-6
7. Je,Elohim huyasikia maombi ya watakatifu? 1 Peter 3:12

**SOMO LA WATOTO LA FEBRUARY 15, 2025**
**KUTII**
**Somo kuu : I Samueli 15:1-35**
**Fungu la kukariri : 1 Samueli 15:22**

1. Elohim huona uasi kivipi? 1 Samueli 15 :23
2. Ili tumfurahishe Elohim twafaa tufanye vipi? 1 Samueli 15:22
3. Je,manabii walimtii Elohim? 1 Samueli 3:10,Hosea 4:2-3
4. Je,Masihi alipata kibari cha kupendwa na Elohim pamoja na watu kwa sababu ya kuwa mtiifu? Luka 2:52
5. Je,watakatifu wameamuriwa kutii Elohim kwa njia ya kuzitunza amri zake? Ufunuo

14:12
6. Ni kwa njia ipi twaweza kuonyesha upendo wetu na utiifu kwa Elohim? Yohana 14:15
7. Je,watoto wameshauriwa kuwatii wszazi wao? Waefeso 6:1

**SOMO LA WATOTO LA FEBRUARY 22, 2025**
**KUZALIWA KWA MASIHI**
**Somo kuu: Luka 2**
**Fungu la kukariri : Luka 2:52**

1. Je,manabii walijua Mahali ambapo Masihi angezaliwa? Mika 5:2,Mathayo 2:5
2. Nani alitaka kumuua Masihi? Luka 2:1
3. Nani alikuwa mama yake? Mathayo 1:18
4. Kwa nini Masihi na wazazi wake walienda Misiri? Mathayo 2:13-14
5. Ni lini walirudi kutoka Misiri? Mathayo 2:19-21
6. Ni katika Mji upi waliishi baada ya kutoka Misiri? Mathayo 2:23
7. Katika utotoni wake, je alikuwa ana watii wazazi wake na Elohim? Luka 2:52

**SOMO LA WATOTO LA MARCH 1, 2025**
**IMANI**
**Somo kuu : Waebrania 11:1-40**
**Fungu la kukariri : Waebrania 11:6**

1. Imani ni nini? Waebrania 11:1
2. Je, twaweza kumfurahisha Elohim pasipo kuwa na Imani? Waebrania 11:6
3. Ni nini Nabii Habakuki amenena kuhusu Imani? Habakkuki 2:4
4. Ni nani Masihi alimpongeza kwa sababu ya Imani yake kubwa? Mathayo 8:8-10
5. Je, Masihi aliwaamuru watu wawe na Imani kwake Elohim? Marko 11:22
6. Wakati mwanamke mmoja mugonjwa alipomgusa Masihi je Imani yake ilimponya? Luka 8:47-48

7. Je, imani inahitajika ili Mtu awe mtakatifu? Ufunuo 14:12

**SOMO LA WATOTO LA MARCH 8, 2025**

**UBATIZO**
**Somo kuu : Yohana 3:1-12**
**Fungu la kukariri : Yohana 3:3**

1. Masihi alinena vipi kuhusu ubatizo? Yohana 3:3
2. Mitume walibatiza vipi? Matendo ya Mitume 2:38,19:5
3. Je, Masihi alibatiza watoto? Mathayo 19:13-15

4. Masihi alipokuwa mtoto, je alibatizwa? Luka 2:25-29
5. Mtu hubatizwa kwa njia gani? Mathayo 3:16,Warumi 6:3-4
6. Ni aina ngapi za ubatizo hupatikana katika bibilia? Waefeso 4:5
7. Baada ya kubatizwa twaweza kutenda dhambi kisha tubatizwe tena? Waebrania 10:26-29

**SOMO LA WATOTO LA MARCH 15, 2025**
**UZIMA WA MILELE**
**Somo kuu: Yohana 17**
**Fungu la kukariri : Yohana 3:16**

1. Ni kwa nini Elohim alimtuma mwanawe wake aje ulimwenguni? Yohana 3:16
2. Nini ahadi ya Masihi kwetu? 1 Yohana 2:25
3. Je, mtu anaye waua wengi e ana uzima wa milele? 1 Yohana 3:15
4. Ni swali gani mtu moja alimuuliza Masihi kuhusu uzima wa milele? Mathayo 19:16
5. Jibu la Masihi, lilikuwa lipi? Mathayo 19:17
6. Tukimuamini Masihi, je tutapata uzima wa milele? 1 Yohana 3:15
7. Nini karama ya Elohim kwa waliomwamini? Warumi 6:23.

**SOMO LA WATOTO LA MARCH 22,2025**
**KUJA KWA MASIHI MARA YA PILI**
**Somo kuu : Matendo ya Mitume 1:1-12**
**Fungu la kukariri : Matendo ya Mitume 1:11**

1. Je, Masihi atarudi tena Mara ya pili? Waebrania 9:28
2. Je,aliahidi kuja tena mara ya pili? Matendo ya Mitume :1:11
3. Ni nini alimwambia mmoja wa mitume wake kuhusu Kuja kwake mara ya pili? Yohana 14:1-3
4. Atakapokuja mara ya pili, je tutatawala naye? Ufunuo 20:4
5. Nabii Zekaria amenena vipi kuhusu kuja mara ya pili kwake Masihi? Zekaria 14:1-9

6. Watu wote wenye watakuwa hai atakaporudi mara ya pili, je wote watamuona? Ufunuo 1:7

7. Nini kitafanyika kwa wale waliokufa wakiwa ndani yake? 1 Wathesalonike 4:16-17

**SOMO LA WATOTO LA MARCH 29, 2025**
**MJI ULE MTAKATIFU (YERUSALEMU MPYA)**
**Somo kuu : Ufunuo 21:1-22**
**Fungu la kukariri : Ufunuo 21:2**

1. Nani aliona Mji ule mtakatifu ukishuka duniani? Ufunuo 21:2
2. Ni milango ngapi itakuwa katika Mji ule mtakatifu? Ufunuo 21:12
3. Ni lipi jina la mji wa Elohim? Ufunuo 3:12
4. Je,mwandishi wa waraka wa waebrania alinena kuhusu mji huu? Waebrania 13:14
5. Nani Mjenzi wa mji huu? Waebrania 11:10
6. Ni nini kinahitajika ili mtu aingie katika mji mtakatifu? Ufunuo 22:14
7. Je,watu waovu wataingia katika mji mtakatifu? Ufunuo 21:27, 22:15